HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MPANGO WA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MSITU WA KIJIJI CHA KIKOLE

MPANGO WA USIMAMIZI UMEANDALIWA NA KIJIJI CHA KIKOLE.

YALIYOMO

1. Utangulizi ---- 3
1.1 Madhumuni Na Malengo Ya Usimamizi Wa Misitu ---- 3
1.1.1 Madhumuni ---- 3
1.1.2 Malengo Ya Kutunza Msitu ---- 3
2. Maelezo Ya Jumla Kuhusu Msitu ---- 4
2.1 Umiliki Wa Msitu ---- 4
2.2 Mahali Msitu Ulipo Na Ukubwa Wake ---- 4
2.3 Hali Ya Mvua ---- 4
2.4 Njia Za Mawasiliano ---- 4
2.5 Aina Ya Udongo ---- 4
2.6 Uoto Wa Asili ---- 4
3. Rasilimali Zilizopo Kwenye Msitu ---- 5
3.1 Mazao Ya Msitu. ---- 5
3.1.1 Aina Ya Miti. ---- 5
3.1.2 Mazao Mengine ---- 5
3.1.3 Wanyama Wanaopatikana Katika Msitu Huu ---- 5
3.1.4 Aina Za Ndege ---- 5
3.1.5 Aina Ya Nyoka Na Mijusi ---- 5
3.2 Ukusanyaji Wa Takwimu Za Mazao Ya Misitu. ---- 5
3.2.1 3.2.1 Maandalizi. ---- 6
3.3 Uchambuzi Wa Takwimu ---- 6
3.4 Matokeo Ya Uchambuzi ---- 7
3.4.1 3.4.1 Upatikanaji Wa Zao La Mbao Katika Msitu Wa Jamii Kikole Umeainishwa Katika Jedwali ---- 7
4. Shughuli Za Kuendeleza Na Kutunza Msitu Wa Jamii Kijiji Cha Kikole. ---- 9
4.1 Mikakati Ya Jumla Ya Kuendeleza Msitu ---- 9
4.2 Upandaji Wa Miti Na Utunzaji Wa Miti Ya Mbao Na Magogo. ---- 9
4.3 Ulinzi Wa Msitu. ---- 9
4.4 Ushirikishwaji Wa Jamii Katika Ulinzi Wa Msitu ---- 10
4.5 Walinzi Wa Doria ---- 10
4.6 Udhibiti Wa Moto ---- 10
4.7 Mpango Wa Matumizi Wa Mazao Ya Msitu. ---- 10
5. Wajibu Na Majukumu Ya Wadau Wa Misitu ---- 11
5.1 Wajibu Na Majukumu Ya Kila Mdau ---- 11
5.1.1 Serikali Kuu ---- 11
5.1.2 Halmashauri Ya Wilaya. ---- 11
5.1.3 Serikali Ya Kijiji ---- 11
5.1.4 Kamati Ya Maliasili ---- 11
5.1.5 Mgawanyo Wa Mapato Yatokanayo Na Mazao Ya Msitu. ---- 12
6. Masharti Ya Matumizi Ya Msitu Na Mazao Ya Msitu ---- 13
6.1 Matumizi Yatakayoruhusiwa Bure. ---- 13
6.2 Matumizi Yatakayoruhusiwa Kwa Leseni/Ushuru. ---- 13
6.3 Mazao Ya Kulipia Ushuru. ---- 13
6.4 Mazao Yatakayovunwa Kwa Leseni. ---- 13
6.5 Matumizi Yasiyoruhusiwa Ndani Ya Msitu. ---- 13
6.6 Sheria Ndogo Za Kijiji. ---- 13
6.7 Matumizi Mengine. ---- 14
7. Mapato Na Matumizi Ya Msitu. ---- 15
7.1 Vyanzo Vya Mapato. ---- 15
7.1.1 Matumizi ---- 15
7.1.2 Shughuli Za Kuendeleza Na Kutunza Misitu Na Huduma Za Jamii ---- 15
7.1.3 Vitabu Muhimu Kwa Ajili Ya Kutunza Kumbukumbu ---- 15

7.2 Utoaji Wa Taarifa Ya Mapato/Matumizi Ya Fedha. ---------- 15
7.3 Usimamizi Wa Fedha ---------- 15
8. Ufuatiliaji Wa Tathmini. ---------- 17
8.1 Ufuatiliaji. ---------- 17
8.1.1 Shughuli Zitakazofuatiliwa ---------- 17
8.1.2 Tathmini Shirikishi. ---------- 17
KIAMBATANISHO: A ---------- 18
KIAMBATANISHO: B---------- 21

Kiambatisho: C ---------- 23

SURA YA KWANZA

1. UTANGULIZI

Mkakati wa usimamizi shirikishi wa misitu unaipa jamii sehemu kubwa ya utekelezaji na manufaa. Ni mkakati unaolenga katika kuyaweka maeneo mengi ya misitu chini ya usimamizi madhubuti na endelevu. Utaratibu huu unatumika kwenye misitu isiyohifadhiwa ndani ya kijiji au ardhi huria na misitu ya hifadhi (aidha ya Serikali kuu, Serikali za mitaa au Serikali za vijiji). Katika mkakati huu mgawanyo wa majukumu huwekwa bayana.

Mpango huu wa Taifa wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu umeanzishwa kisheria, ambapo umerasimishwa na vyombo vifuatavyo; Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998, Mpango wa Taifa wa misitu wa mwaka 2001, Mwongozo wa usimamizi shirikishi wa misitu Tanzania wa mwaka 2001, Sheria ya misitu na.14 ya mwaka 2002, na kanuni za uendeshaji wa misitu 2004.

Mpango huu wa usimamizi shirikishi wa msitu wa jamii wa Kijiji cha Kikole umeandaliwa na kamati ya Maliasili ya kijiji wakishirikiana na timu ya wataalamu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa. Mpango huu ulidhibitishwa na Halmashauri ya kijiji na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji.

Mkakati wa ushirikishwaji wa jamii katika usimamizi wa misitu ulielezwa kwa njia ya vikao na mafunzo mbalimbali kwa viongozi na wanajamii kwa ujumla na kukubalika na walio wengi, hivyo jamii ya kijiji cha Kikole imeandaa mikakati ya usimamizi wa rasilimali za msitu wao. Mikakati hii imeelezwa kwa undani zaidi katika kabrasha hili la mpango wa usimamizi shirikishi wa msitu. Mpango huu umefafanua na kuweka bayana shughuli zote zitakazofanyika katika kipindi chote cha kutunza, kusimamia na kutumia msitu. Mpango huu pia umeeleza kanuni na masharti ya matumizi ya msitu na mazao yake ili kuwa na matumizi endelevu. Mambo mengine yaliyoelezwa kwenye mpango huu ni pamoja na wajibu na majukumu ya wadau wa misitu, mgawanyo wa mapato yatokanayo na msitu kwa wadau hao kutokana na majukumu yao. Vilevile mpango huu umeeleza njia zitakazotumika katika kufuatilia na kutathmini shughuli zilizopangwa. Ili masharti ya matumizi ya msitu yaweze kufuatwa ipasavyo, kijiji kimetunga sheria ndogondogo za utunzaji na utumiaji wa msitu. Kwa kuwa kijiji kitakuwa kinatayarisha mpango wa kazi wa kila mwaka, mpango kazi huo pia utawekwa kama kiambatanisho kwenye mpango huu.

1.1 Madhumuni Na Malengo Ya Usimamizi Wa Misitu

1.1.1 Madhumuni

- Kijiji kimetenga eneo la msitu kukidhi mahitaji ya mazao ya misitu kwa matumizi ya sasa na vizazi vijavyo**.**
- Kutunza, kusimamia na kutumia rasilimali za misitu kiuendelevu kwa ajili ya kuhifadhi bionuai ya misitu na kuboresha uchumi wa jamii ya kijiji cha Kikole.

1.1.2 Malengo Ya Kutunza Msitu

- Ifikapo mwaka 2010 jamii ya Kikole itakuwa imejengewa uwezo endelevu wa kutunza, kusimamia na kutumia rasilimali za mazao ya msitu kwa asilimia 40%
- Hekta 450 za msitu wa jamii wa kijiji cha Kikole zitakuwa zimetunzwa na kusimamiwa kwa kiwango cha 50% ifikapo mwaka 2010.
- Msitu wa kijiji cha Kikole utakuwa umeboresha hali ya uchumi kwa wanajamii kwa kiasi kidogo ifikapo mwaka 2010.

SURA YA PILI

2. MAELEZO YA JUMLA KUHUSU MSITU

2.1 Umiliki Wa Msitu

Msitu wa jamii unamilikiwa na serikali ya kijiji cha Kikole na umetengwa kuwa msitu wa hifadhi mwaka 2004. Msitu umepimwa na kuchorewa ramani.

Kamati ya maliasili ya kijiji iliyoundwa na mkutano mkuu wa kijiji ndio meneja wa msitu.

2.2 Mahali Msitu Ulipo Na Ukubwa Wake

Msitu wa jamii wa Kikole upo katika kijiji cha Kikole, kata ya Kikole, tarafa ya Pwani Wilayani Kilwa.

Msitu huu umepakana na kijiji cha Mitole upande wa magharibi, upande wa mashariki kijiji cha Kikole, upande wa kusini umepakana na msitu hifadhi wa Taifa Mitarurena upande wa kaskazini umepakana na Kikole.

Msitu wa jamii wa kijiji cha Kikole una eneo la hekta 450 na sehemu kubwa ya msitu ni miinuko.

2.3 Hali Ya Mvua

Kuna kipindi kimoja kikubwa cha mvua. Mvua ni nyingi kipindi cha masika nacho huwa kinaanzia mwezi wa Desemba hadi mwezi wa Mei.

2.4 Njia Za Mawasiliano

Msitu wa jamii kijiji cha Kikole unaweza kufikiwa kwa kutumia njia ya;

a) Nangurukuru-Mgeregere-Kikole kwa wakati wa kiangazi

b) Wakati wa masika msitu wa jamii unaweza kufikiwa kwa kutumia njia ya Nangurukuru-Migeregere-Mbate-kwa njia ya Liwale hadi kwenye kibao cha Shule ya Sekondari ya kata ya Kikole.

2.5 Aina Ya Udongo

Kuna aina mbalimbali za udongo katika msitu wa jamii wa kijiji cha Kikole ;

-Mchanga unapatikana njengani

-Mfinyanzi unapatikana ulamboni

-Mchanganyiko wa mfinyanzi na mawe unapatikana mlimani.

2.6 Uoto Wa Asili

Msitu wa jamii wa Kikole una aina ya uoto wa miombo (nyasi nyingi na vichaka, pamoja na miti iliyotawala zaidi ni miti ya mipingo na mianzi).

SURA YA TATU

3. RASILIMALI ZILIZOPO KWENYE MSITU

3.1 Mazao Ya Msitu.

3.1.1 Aina Ya Miti.

Tathimini shirikishi ya mazao ya msitu iliyofanyika mwezi oktoba 2004 ilionyesha kuwa msitu una jumla ya aina ya miti 52 ambayo inaweza kutumika kwa matumizi mbalimbali kama mbao, majengo, fito, mkaa, kuni, madawa, matunda. Miti ya mbao inayopatikana katika msitu huu ni mpingo,mkunya, mkongo, mninga, mpangapanga, myombo, mtondo, mhembeti, mvule, mkarati, msufipori na mlondondo. Miti ya majengo ni mnepa, msumari, mkuyakuya, mtembele, mpugupugu, mjongoo, mkundekunde, msekese, mkandapori, kingonogo, mkiu, mkia, mtandawala, mpalapala, mngamba, mngulunguya, mtopetope, mkokonaimba, msenjele, mlambunju, mchuluchulu, mkamulamunda, mchekele, mbilia, mkarakawa, msolo. Miti ya matunda ni , mtopetope, mngulunguya, mpinji, mbalubalu, mhilu, mkunya na mgongo. Miti ya kamba ni mkunya, mnepa, mtondo, myombo, mkiu, msekeseke.

3.1.2 Mazao Mengine

Mazao mengine yanayopatikana katika msitu wa jamii ni uyoga, mg'oka**,** ulanga (chakula), lukokoti, angai, na nakatukwe (mboga). Uyoga ni zao linalovunwa sana kuliko zao lingine wakati wa msimu wa masika. Aina za uyoga zinazopatikana ni uguyugu, uyoga ndembo, upoa, lunguvale, ugawa wa mbwa, lengangalakate, ugowele, uyoga mbuyu, kitofu, mkwanga, mkobalibu, mpugupugu na ulelema.

3.1.3 Wanyama Wanaopatikana Katika Msitu Huu

Wanyama wanaopatikana katika msitu huu ni ndandala, nyati, kongoni,mbawala, mbarapi, ndope, ngolombwe, mbunju, ndogolo, nungu, ngiri, sungura, nyani, nguruwe, kima, nguchilo, tumbili, simba, chui, mkwamda, mjusi, fisi, tembo, swala, kobe na kungusi.

3.1.4 Aina Za Ndege

Aina za ndege wanaopatikana katika msitu huu ni kanga, hondohondo, ngukiwe, kololo, kwelekwese, chiriku, tondohole, kituku, kichapi, njiwa, koekoe, kusese, namkoko, ngalukulu, bwanda, ngwihili, segu, nditi, namgong'onda, mwingo, kindololo, tambusi, nyanga, mwewe, kitotola, kapungu, mbayuwayu, nandambala, njegeya, bangobongo, ngwalu, ninga,tipitipi na tyole.

3.1.5 Aina Ya Nyoka Na Mijusi

Aina za nyoka wanaopatikana katika msitu huu ni chatu, boma, ndemela, mnalu, ndungulu, mbito, mpilato, lulukuti, nyoka ufuta, mlulu, nachiku, kipitahalo na cobra.

Mijusi inayopatikana kwenye msitu ni mkwanguru, kengenamkwangula, kikoyambako, namkoboka, kijengamahuta na mjusimsilamu.

3.2 Ukusanyaji Wa Takwimu Za Mazao Ya Misitu.

Zoezi la uhakiki shirikishi wa mazao ya msitu ukiwepo kuhesabu na kupima mazao ya misitu ni moja kati ya mazoezi muhimu yaliyofanikisha utayarishaji wa mpango huu.

Zoezi hili lilifanyika katika njia kuu tatu

3.2.1 3.2.1 Maandalizi.

(a) Mafunzo
Kamati ya maliasili ya kijiji ilipewa mafunzo ya mbinu rahisi na nyepesi kuzifuata za uhesabuji na upimaji wa mazao ya msitu. Pia mafunzo hayo yalitoa njia rahisi za uchambuzi wa takwimu na namna ya kuzitafsiri kwenye majedwali.

(b) Hojaji, Madodoso na matembezi ya mkato.
Hojaji na madodoso yaliyofanywa kwenye kaya zilizochaguliwa kwa mchanganyiko yalilenga kufahamu mahitaji halisi ya jamii katika kutumia mazao ya misitu.

Aidha hojaji hizo pamoja na matembezi ya mkato ziliwezesha jamii husika kupanga na kuamua aina ya mazao ya kuhesabu na idadi ya vitalu vya uhesabuji (vitalu viwakilishi)

(c) Mbinu za uhesabuji wa mazao ya misitu
Uhesabuji ulifanyika kwenye vitalu vya sampuli ambavyo idadi yake ilipatikana kwa kutumia kanuni ifuatayo;

$$\text{Idadi ya vitalu} = \text{Eneo} \frac{\text{la msitu kwa ha x \% ya kiwango cha uhakika}}{\text{Eneo la kitalu kwa ha}}$$

Kiwango cha % kilichotumika kupata vitalu vya uwakilishi ni 0.05.

Kiwango hicho kilichaguliwa kutokana na ufinyu wa muda na shughuli nyingi za kilimo zilizokuwa zinawakabili wanakijiji. Hivyo vitalu vilivyopatikana kutokana na kiwango hicho katika eneo la hekta 450 la msitu vilikuwa vitalu 27. Hata hivyo kiwango hicho cha uhakika kilichotumika kilitupatia taarifa muhimu zinazohitajika katika kuandaa mpango huu.

(d) Vitalu vya sampuli
Kila kitalu cha sampuli kilikuwa na umbo la mraba lenye eneo la mita za mraba l00 ($100m^2$)

Umbo la kitalu lilichaguliwa ili kuwawezesha washiriki kuwa na uelewa na ushiriki sawa wakati wa kukusanya takwimu.

Umbali toka kitalu kimoja na kingine ilikuwa mita 400.

Umbali kutoka mstari wa kufikiriwa hadi mwingine ni mita 500.

(e) Uhesabuji na upimaji wa mazao ya misitu
Mimea mbalimbali ndani ya kitalu cha sampuli ilitambuliwa kwa majina ya kienyeji. Machipukizi ya mimea yote yalihesabiwa na miti yenye unene wa kuanzia sentimeta 16 ilipimwa. Utambuzi wa mimea yote ulifanyika kwa wadau husika wenye ufahamu wa mimea hiyo.

Vifaa vilivyotumika ni pamoja; futi kamba, kamba, kipima pembe, G.P.S, dira (compass), penseli, vigingi, fomu za kujaza na kamba iliyotumika ilikuwa na urefu wa mita 40.

3.3 Uchambuzi Wa Takwimu

Uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa katika vitalu kufuatilia zoezi la muda mrefu la uhakiki shirikishi wa mazao ya misitu takwimu zilifanyiwa uchambuzi wa kina. Miti na mazao mengine yatokanayo na misitu yalichambuliwa kutokana na matumizi kama mbao, majengo, fito, madawa, matunda, mkaa, mboga, kamba, kuni na vinyago.

3.4 Matokeo Ya Uchambuzi

3.4.1 3.4.1 Upatikanaji Wa Zao La Mbao Katika Msitu Wa Jamii Kikole Umeainishwa Katika Jedwali



Kutokana na jedwali hilo hapo juu miti aina ya mpingo inaongoza ikifuatiwa na miti aina ya mpangapanga. Mpingo imeonekana kuwa na upatikanaji mkubwa katika msitu huu. Kwa ujumla msitu huu wa jamii wa kijiji cha Kikole hauna miti ya kuweza kukidhi mahitaji. Hivyo maoni yetu tunatarajia kupanda miti ya mbao pamoja na utunzaji wa machipukizi dhidi ya moto ili kuongeza uwingi wa miti hiyo kuweza kutosheleza mahitaji ya mazao ya msitu kwa sasa na vizazi vijavyo.

Jedwali na 2. Mgawanyiko wa miti ya mbao katika madaraja ya unene.



Jedwali hapo juu linaonyesha kuwa kuna upungufu wa miti katika madaraja ya juu (150-199.9, na 200-249.9)

Hata hivyo jamii ya Kikole imeamua itafanya uvunaji wa miti ya mipingo iliyokomaa katika mwaka 2006 na hakutakuwepo na uvunaji wa miti aina nyingine ya mbao kutokana na upungufu ulioko wa miti hiyo ndani ya msitu wa jamii.

Kwa upande wa miti ya majengo na fito itaendelea kuvunwa toka kwenye msitu huo kwa kutumia taratibu maalumu za uvunaji endelevu.

Jedwali na 3. Upatikanaji wa miti ya majengo kwa matumizi mbalimbali



Kutokana na jedwali hilo hapo juu zao la fito zinapatikana kwa wingi zaidi ikifuatiwa na zao la majengo. Zao la nguzo limeonekana linapatikana kwa kiasi kidogo zaidi, hivyo kuna umuhimu wa kuchukua tahadhari ili kuongeza zao hilo.



Jedwali na 4;

Upatikanaji wa zao la majengo

Jedwali linaonyesha kuwa zao la mkiu, kingonogo,na mtandawala linapatikana kwa wingi. Upatikanaji wa miti mingine ya majengo ni michache nayo ni mkarakawa, mnjekele, kimbilia, mkandaa pori, mgamba, mjongoo, mkia, mkuyakuyana mkudekunde.

SURA YA NNE.

4. SHUGHULI ZA KUENDELEZA NA KUTUNZA MSITU WA JAMII KIJIJI CHA KIKOLE.

Kutokana na msitu kuwa na uoto wa aina mbalimbali, msitu mzima una maeneo mawili ya utunzaji nayo ni eneo la Ruhunda na eneo la Mpitaniki.

Mambo yatakayoangaliwa au kupewa umuhimu ni;

-Kupanda miti sehemu za wazi.

-Kulinda msitu kwa kutengeneza kinga za moto, kufanya doria za mara kwa mara (wiki mara mbili) pamoja na kuandaa matumizi endelevu ya misitu.

4.1 Mikakati Ya Jumla Ya Kuendeleza Msitu

Katika kuendeleza msitu mikakati ya jumla itakayofanyika ndani ya msitu ni kama ifuatavyo.

-Kudhibiti uchomaji moto.

-Uwekaji kinga moto.

-Kufanya doria za mara kwa mara ili kudhibiti uvunaji holela na uharibifu mwingine wa msitu.

-Kuthibiti kilimo cha aina yeyote na makazi ndani ya msitu.

-Kuthibiti kufanya uchungaji wa mifugo ndani ya msitu.

-Kutakuwepo utaratibu utakaoandaliwa wa kuingia msituni.

4.2 Upandaji Wa Miti Na Utunzaji Wa Miti Ya Mbao Na Magogo.

Upandaji wa miti ya mbao na magogo na utunzaji wa machipukizi utategemea nauwepo wa machipukizi ya miti kutokana na uvunaji wa miti usioendelevu uliofanyika kipindi kilichopita na uchomaji moto ovyo. Miti ya mbao itakayotiliwa mkazo kupandwa ni miti aina ya mvule, mningajangwa, mkongo, mtondo, mwebeti, mkarati, msufipori na mlondondo.

Miti hiyo imeonekana ina umuhimu wa kuongezwa kwa kuyatunza machipukizi pamoja na kupanda miche kutokana na uchache wa miti hiyo kama ilivyoonyesha kipindi cha uhakiki.

Miti ya majengo iliyoonekana kupatikana kwa wingi nayo ni; mkiu mtandawala, kingonogo, mngulunguya, msekeseke, mtopetope, mpugupugu na mnepa. Machipukizi ya miti yalionekana mengi hivyo uchomaji moto udhibitiwe ili kuruhusu ukuaji wa machipukizi.

4.3 Ulinzi Wa Msitu.

Msitu utakuwa chini ya serikali ya kijiji na kulindwa na wanajamii. Kutakuwa na kikosi cha doria ambacho kitakuwa na watu wafuatao

- Kamanda wa doria 1
- Wanakamati wa maliasili 3
- Wanajamii 2

Kikosi hiki kitatoa taarifa kwa kamati ya maliasili baada ya kutekeleza majukumu. Doria zitakuwa zikifanywa mara nne kwa mwezi. Kijiji kitatoa posho kwa kwa wana doria pale hali itakaporuhusu. Kikosi hiki cha doria kitabadilishwa kila baada ya miezi sita (6), isipokuwa kamanda. Pia kamati hii ya doria itabadilishwa na mkutano mkuu wa kijiji.

4.4 Ushirikishwaji Wa Jamii Katika Ulinzi Wa Msitu

Jamii ya Kikole itawajibika kulinda msitu huo. Kila mwanajamii anatakiwa kutoa taarifa pale anapoona kunatofauti na taarifa itolewe kwa;

- Serikali ya kijiji.
- Kamati ya maliasili.
- Kikosi cha doria.

Mwanajamii atatoa taarifa ya uharibifu wa msitu huo na kuelezea aina ya uharibifu uliofanyika ni wa aina gani mfano;

- Upasuaji wa mbao haramu.
- Majangili
- Moto
- Ukataji wa magogo
- Uchomaji wa mkaa n.k

Kamati ya maliasili itasimamia na kuratibu shughuli zote za doria kwa kupanga zamu za askari wa doria.

4.5 Walinzi Wa Doria

Wajumbe wote wa kamati ya doria watachaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji na wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo;

- Awe amepitia mafunzo ya mgambo.
- Awe mzoefu wa kutembea msituni.
- Awe jasiri na mwenye nguvu.
- Awe mwaminifu na mwenye kujituma.
- Awe mpenda mazingira.

4.6 Udhibiti Wa Moto

Udhibiti wa moto utafanyika kwa kutengeneza barabara za kinga za moto kuzunguka msitu wote hasa baada ya mvua za mwisho kunyesha.

4.7 Mpango Wa Matumizi Wa Mazao Ya Msitu.

Kutokana na takwimu za uhesabuji miti imeonekana kuwa idadi ya miti ya mbao ni michache, hivyo jamii imesitisha uvunaji wa miti ya mbao pamoja na magogo ili kutoa nafasi kwa miti iliyopo kukomaa. Hata hivyo uvunaji wa mazao mengine kama mpingo na mianzi unaweza kufanyika kwani miti hii imeonekana kuwa ipo ya kutosha.

SURA YA TANO

5. WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU WA MISITU

Wadau wa msitu wa jamii kijiji cha kikole ni;

- Serikali Kuu.
- Halmashuri ya Wilaya.
- Wanajamii wa Kijiji cha Kikole.-

5.1 Wajibu Na Majukumu Ya Kila Mdau

5.1.1 Serikali Kuu

-Kubuni na kuandaa sera na kutoa mwongozo wa misitu na kushirikisha jamii zinazoishi kandokando ya misitu kuitunza na kuindeleza kwa manufaa ya sasa na baadaye.

-Kutoa wataalam inapobidi.

5.1.2 Halmashauri Ya Wilaya.

-Kutoa wawezeshaji na wataalam wa kutoa mafunzo juu ya misitu ya jamii kwa kamati ya maliasili na jamii.

-Kutoa msaada kwa kutafuta soko la mazao ya misitu.

-Kusimamia na kutatua migogoro pindi itakapotokea.

-Kutoa msaada wa mbegu pamoja na utaalamu inapobidi.

5.1.3 Serikali Ya Kijiji

Majukumu ya Serikali ni kama ifuatavyo;

-Kushiriki kwa kikamilifu katika kutunza na kulinda msitu.

-Kutambua matatizo yanayowakabili wanakamati na kuyatatua.

-Ni msimamizi mkuu wa shughuli zote za utunzaji wa msitu pamoja na mazingira.

-Kudhibiti mapato yote yatokanayo na msitu.

-Kuwapa taarifa wadau wote waliopo ndani ya kijiji na nje ya kijiji zinazohusu shughuli za msitu.

-Kuwa na uwezo wa kumsimamisha mwanakamati endapo ataenda kinyume na utaratibu wa kazi yake.

-Kupokea taarifa ya uharibifu wa msitu toka kwa wanajamii na kuzifanyia kazi.

-Kufuatilia vibali vyote vilivyotolewa na kamati ya maliasili vya uvunaji wa mazao ya misitu.

-Kuidhinisha matumizi na mapato ya fedha kwa wajumbe wa serikali ya kijiji kwa ajili ya matumizi ya msitu.

5.1.4 Kamati Ya Maliasili

- Kusimamia na kuratibu shughuli zote za msitu.
- Kutoa vibali vya uvunaji wa mazao ya msitu.
- Kufuatilia kwa karibu shughuli zote kama vile upandaji wa miti, ukusanyaji wa mazao ya msitu na kutunza kumbukumbu za msitu.
- Kusimamia na kufuatilia uvunaji.
- Kupendekeza sheria ndogondogo za kijiji kuhusu msitu.
- Kutoa taarifa za uharibifu wa msitu kwa serikali ya kijiji.
- Kubuni miradi ya kiuchumi ya jamii.

5.1.5 Mgawanyo Wa Mapato Yatokanayo Na Mazao Ya Msitu.

Mgawanyo wa mapato yatokanayo na mazao ya msitu kati ya Serikali ya Kijiji na Halmashauri ya Wilaya. Mgawanyo huu utazingatia ni nani mwenye mali na ni nani mwenye majukumu makubwa zaidi katika kuendeleza msitu.

SURA YA SITA

6. MASHARTI YA MATUMIZI YA MSITU NA MAZAO YA MSITU

Watumiaji wa msitu watakuwa wanakijiji wenyewe.

Watumiaji wengine wanatakiwa kutumia taratibu ya kupata kibali kilichotolewa na kijiji.

Kwa wanajamii wa Kikole itawabidi kuchangia mfuko wa maendeleo ya kijiji kwa baadhi ya mazao na mazao mengine yatatolewa bure pamoja na kiasi kitakachochukuliwa kwa siku maalum zitakazopangwa.

6.1 Matumizi Yatakayoruhusiwa Bure.

Matumizi ya mazao madogo kama uyoga, mboga, matunda yote ya msitu nyasi na kuni kavu.

Kwa mazao ya madawa na kamba yataruhusiwa kwa matumizi ya binafsi tu na kama ni biashara itabidi kulipia.

6.2 Matumizi Yatakayoruhusiwa Kwa Leseni/Ushuru.

Kutundika mizinga ndani ya msitu.

Kuingia ndani ya msitu kwa ajili ya kufanya mafunzo, utafiti pamoja na utalii.

Kutumia mazao ya misitu ajili ya shughuli za maendeleo ya huduma za jamii kama ukarabati/ujenzi wa shule, hospitali n.k.

6.3 Mazao Ya Kulipia Ushuru.

Mazao ambayo yatahitaji kulipiwa ushuru ni boriti, kongowele, mianzi na tungo. Kwa matumizi ya nyumbani mwanajamii atalipa robo ya kiwango kitakachokubalika.

6.4 Mazao Yatakayovunwa Kwa Leseni.

Mazao yatakayovunwa kwa leseni ni mbao, magogo, wanyama pori mianzi na nguzo. Uvunaji wa mazao hayo hautatofautisha mfanyabiashara toka nje ya kijiji au mwanakijiji.

6.5 Matumizi Yasiyoruhusiwa Ndani Ya Msitu.

- Kuchuna magamba ya miti kwa ajili ya kamba.
- Kuchuna magome kwa ajili ya matumizi mbalimbali
- Kuchoma moto ovyo ndani ya msitu.
- Kilimo ndani ya msitu.
- Kufanya makazi ndani ya msitu.
- Kuchunga mifugo ndani ya msitu.
- Kuchoma mkaa.
- Kutega na kuwinda wanyama na ndege kwenye msitu.

6.6 Sheria Ndogo Za Kijiji.

Kijiji kimetunga sheria ndogo za kijiji zitakazosaidia mpango huu wa usimamizi shirikishi wa msitu kuwa na nguvu za kisheria. (Kama ilivyoainishwa kwenye kiambatanisho A)

6.7 Matumizi Mengine.

- Kufanya mafunzo ndani ya msitu ni Shs 10,000/= kwa kundi zima
- Kufanya tafiti ada itakayolipwa ni Shs 3,000/= kwa siku, watakaowaongoza watalipwa 5,000/= kila mmoja
- Kufanya utalii ndani ya msitu Shs 10,000/= kila mtalii mmoja na waongozaji watalipwa Shs 7,000/= kila mmoja kwa siku moja.
- Watakaokiuka masharti ya msitu watatozwa faini kiasi kilichochapishwa katika sheria ndogo.

SURA YA SABA

7. MAPATO NA MATUMIZI YA MSITU.

7.1 Vyanzo Vya Mapato.

Kutakuwa na vyanzo vya mapato yatokanayo na mazao ya msitu kama;

- Mauzo ya mazao ya msitu.
- Ada kutokana na mafunzo, tafiti mbalimbali na utalii.
- Ushuru.
- Leseni.
- Faini za wahalifu.

7.1.1 Matumizi

Kipaumbele cha matumizi ya mapato yatokanayo na msitu yataelekezwa katika shughuli za kuendeleza msitu kama zitakavyokuwa zimepangwa katika mpango wa mwaka. Mapato mengine yatatumika katika huduma za jamii.

Matumizi yatokanayo na msitu kwa upande wa kijiji yatapangwa na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji. Kijiji kitatenga fedha za kutosha kuendesha shughuli za maliasili za kijiji ambapo matumizi hayo yatatokana na mpango kazi ulioandaliwa wa kila mwaka.

7.1.2 Shughuli Za Kuendeleza Na Kutunza Misitu Na Huduma Za Jamii

- Kulinda msitu (doria za mara kwa mara)
- Kupanda miti maeneo ya wazi msituni.
- Kutengeneza barabara za kuzuia moto wakati wa kiangazi.
- Kukusanya mapato na kuandaa matumizi kwa ajili ya kuendeleza msitu na huduma ya jamii.

7.1.3 Vitabu Muhimu Kwa Ajili Ya Kutunza Kumbukumbu

- Daftari ya fedha.
- Stakabadhi ya fedha.
- Hati ya malipo.
- Daftari la mapato na matumizi (Ledger)
- Kitabu kwa ajili ya wahalifu.
- Kitabu cha kumbukumbu za kila siku za vikao.
- Kitabu cha wageni wanaokuja kutembelea msitu.
- Vifaa vya ofisi.

7.2 Utoaji Wa Taarifa Ya Mapato/Matumizi Ya Fedha.

Serikali ya kijiji itakuwa na wajibu kukusanya mapato yote yatokanayo na msitu**.** Hata hivyo serikali ya kijiji inaweza kuidhinisha ukusanyaji wa mapato kwenye kamati ya maliasili ya kijiji. Kamati haina budi kutunza kumbukumbu zote za mapato na matumizi ya fedha. Kamati itatoa taarifa ya fedha kila mwezi kwa serikali ya kijiji na serikali ya kijiji itatoa tarifa kwa Mkutano Mkuu wa Kijiji kila baada ya miezi mitatu.

7.3 Usimamizi Wa Fedha

Fedha zote zitakazopatikana kutokana na mapato ya msitu zitatunzwa benki. Kutafunguliwa akaunti ya usimamizi shirikishi wa hifadhi ya msitu wa jamii wa kijiji cha Kikole na kutakuwa na watia sahihi maalum wanne.

Kamati ya usimamizi wa fedha wajumbe wake ni kama ifuatavyo;

- Mjumbe mmoja kutoka katika kamati ya mipango na fedha ya kijiji.
- Wanakamati wawili kutoka katika kamati ya maliasili.
- Mtendaji wa kijiji.

SURA YA NANE

8. UFUATILIAJI WA TATHMINI.

8.1 Ufuatiliaji.

Serikali ya kijiji itafuatilia shughuli zote zilizopangwa katika mpango wa kazi wa kila mwaka katika kipindi chote cha miaka mitano. Ufuatiliaji huu utahakikisha kuwa shughuli hizo zimefanyika na kukidhi malengo yaliyowekwa katika kusimamia na kuendeleza msitu.

Malengo haya ni yale yaliyoainishwa katika sura ya kwanza kwenye utangulizi wa mpango huu. Kulingana na mkakati wa uendelezaji na utumiaji wa msitu uliowekwa hakutakuwa na mabadiliko makubwa ya shughuli ya kila mwaka.

8.1.1 Shughuli Zitakazofuatiliwa

Shughuli zitakazofuatiliwa ni kama ifuatavyo;

- Kutengeneza barabara za moto.
- Doria za mara kwa mara.
- Shughuli za kuendeleza msitu (kupanda miti katika maeneo ya wazi na kwenye maeneo huria)
- Ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vibali, leseni na ada zilizotozwa kutokana na uvunaji wa mazao ya msitu.
- Kutunga na kutumia sheria ndogo za kijiji.
- Kutafuta soko la mazao yanayotokana na msitu.
- Kupata mafunzo mazuri ya utumiaji nishati.
- Kupata mafunzo ya ukusanyaji wa mbegu na uoteshaji wa mbegu na upandaji wa miti.
- Kupata mafunzo ya ujasiriamali ya miradi midogodogo ya kiuchumi.

8.1.2 Tathmini Shirikishi.

Kutakuwa na tathmini ya kupima malengo kama ilivyoainishwa kwenye mpango huu.

Kwa madhumuni ya mpango huu tathmini hii itafanyika kila baada ya miaka miwili na nusu na mwishoni mwa miaka mitano

Mpango huu uliandaliwa ili kupima malengo yaliyowekwa na yameainishwa kwenye kiambatanisho “C”.

KIAMBATANISHO: A

SHERIA NDOGO ZA KUTUNZA, KUSIMAMIA NA KUTUMIA RASILIMALI ZA MSITU WA JAMII.

Sheria hizi zimetungwa chini ya kifungu cha 120(1) na163 cha sheria za serikali za mitaa ya mwaka 1982 Na. 7 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2000.

Sheria hizi ziitwe sheria za kutunza, kusimamia na kutumia rasilimali za msitu wa jamii katika kijiji cha Kikole. Sheria hizi zitaanza kutumika kuanzia tarehe……..

Tafsiri ya maneno yaliyotumika katika sheria hizi.

Msitu wa jamii: Maana yake ni eneo la msitu lililotengwa na kijiji lenye miti na uoto wa miti mingine unaomilikiwa na Kijiji cha Kikole.

Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Msitu: Maana yake nikabrasha lenye maelezo ya namna ya kijiji cha Kikole kitakavyotunza, kusimamia, kuendeleza na kutumia rasilimali ya msitu.

Serikali ya kijiji: Maana yake ni Halmashauri ya kijiji cha Kikole.

Mkutano mkuu wa kijiji: Maana yake ni kikao chenye mamlaka na maamuzi ya mwisho katika kijiji cha Kikole kinachohudhuriwa na wanakijiji wote wenye akili timamu na wenye umri usiopungua miaka 18.

Kamati ya maliasili: Maana yake ni kamati iliyoteuliwa na kuundwa na serikali ya kijiji kupitia mkutano mkuu wa kijiji cha Kikole ambayo majukumu yake ni kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazohusu misitu ya jamii na maliasili nyingine zilizopo kwenye kijiji cha Kikole.

Meneja wa msitu : Maana yake ni kamati ya maliasili ya kijiji ambayo kazi yake ni kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazohusu msitu.

Mwanakijiji. Maana yake ni mkazi wa kawaida aliyeandikishwa na serikali ya kijiji cha Kikole.

Kijiji maana yake: Ni eneo ambalo ni makazi ya watu ambalo limewekewa mipaka na serikali kuu na mipaka yake kuainishwa kwenye ramani na kupewa hati miliki.

Maliasili: Maana yake ni vitu vyote vya asili vilivyo hai na visivyohai vilivyopo nchi kavu na baharini.

Mti: Maana yake ni mmea wenye shina lenye unene kuanzia 16cm na kuendelea.

Nguzo: Maana yake ni jengo lenye unene kuanzia 40cm-45cm.

Jengo: Maana yake ni sehemu ya mti iliyonyooka yenye unene wa 25cm-30cm.

Boriti: Maana yake ni sehemu ya mti iliyonyooka yenye unene wa kuanzia 25cm-30cm.

Tungo: Maana yake ni sehemu ya mti iliyonyooka yenye unene kuanzia 16cm-20cm.

Fito: Maana yake ni sehemu ya mti iliyonyooka yenye unene kuanzia 10cm-15cm.

Kongowele: Maana yake ni sehemu ya mti iliyonyooka ambayo inapatikana baada ya mti mkubwa kupasuliwa katikati na kugawanyika katika sehemu.

SEHEMU A: SHERIA NDOGO:

Sheria na.1: Utaratibu wa jumla wa kutumia msitu na mazao ya msitu.

(a) Watu ambao wanaruhusiwa kuingia katika msitu wa jamii wa Kikole kwa shughuli mbalimbali za usimamizi kutokana na taratibu zilizokubalika ni wakazi wa kijiji cha Kikole ni wanakijiji wa Kikole tu.

(b) Watu wengine kutoka nje ya kijiji cha Kikole wataruhusiwa kuingia ndani ya msitu huu wa jamii Kikole kwa vibali maalum endapo watakuwa na shughuli iliyokubalika.

(c) Kwa wale wanakijiji wasiojiweza na ambao wanatambulika na jamii kama vile wagonjwa wa kudumu, walemavu na wazee wanaweza kupata mahitaji ya mazao ya misitu kutoka kwenye msitu wa jamii bure baada ya maombi yao kujadiliwa na kamati husika.

(d) Kwa mazao madogo madogo ambayo ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kama vile uyoga, matunda, mboga pori, ukindu, kuni na madawa ya asili vitaruhusiwa bure isipokuwa kutakuwa na siku maalumu ya kukusanya mazao hayo. Siku hiyo inaweza kubadilika kutokana na matakwa ya jamii.

(e) Mazao yote ambayo ni kwa ajili ya biashara yatavunwa kwa kulipia ushuru na kufuata taratibu zote zilizopangwa kuhusu namna ya kuchukua na kusafirisha mazao hayo.

Sheria na 2; Masharti ya matumizi ya msitu wa jamii wa kijiji.
(i) Matumizi yaliyoruhusiwa bila kibali wala ushuru/ada.
(a) Kutundika mizinga .

(b) Kurina asali bila ya kutumia moto.

(c) Kuvuna mazao ya msitu kwa ajili ya huduma za jamii kama shule na zahanati.

(d) Kuokota kuni kavu kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

(e)Kuchukua kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

(ii) Matumizi yaliyoruhusiwa kwa kutolewa leseni /au ada.
(a) Kuvuna miti kwa ajili ya majengo.

(b) Kuwinda wanyamapori

(c) Kutega ndege.

(d) Kuvuna magogo

(e) Kuingia ndani ya msitu kwa ajili ya kufanya utafiti, mafunzo na utalii.

(f) Kuvuna mazao yaliyotajwa hapo juu kwa ajili ya biashara.

Sheria na 3; **Matumizi yasiyoruhusiwa kufanyika ndani ya msitu wa jamii Kikole.**
(a) Ni marufuku kuanzisha kilimo ndani ya msitu wa jamii.

(b) Ni marufuku kuchoma mkaaa ndani ya msitu wa jamii.

(c) Ni marufuku kuchungia mifugo ndani ya msitu.

(d) Ni marufuku kurina asali kwa kutumia moto na kuangusha miti ndani ya msitu wa jamii.

(f) Ni marufuku kuvuna miti ya mbao yenye unene chini ya 150cm.

(g) Ni marufuku kuvuna magogo ya miti yenye unene chini ya 100cm.

(h) Ni marufuku kuchonga vinu na michi ndani ya msitu wa hifadhi.

(i) Ni marufuku kuchuna magome na kamba ndani ya msitu wa jamii.

(j) Ni marufuku kuchoma moto ndani ya msitu wa jamii.

SEHEMU B: ADHABU.
1. Mtu yeyote atakaye bainika ametenda kosa dhidi ya sheria hizi atatozwa faini isiyozidi fedha taslimu shs 30,000/-.

2. Vifaa vilivyotumika katika ukiukaji wa masharti ya matumizi ya msitu na mazao ya msitu yaliyovunwa vitataifishwa na kuwa mali ya kijiji cha Kikole.

3. Mtu yeyote atakayepuuza au kukataa kulipa faini zilizopangwa katika sheria hizi atafikishwa mahakamani.

4. Mwanakamati yeyote atakaekataa au kutokufika katika ukaguzi wa msitu wa jamii bila sababu yeyote atatozwa faini ya fedha taslim shilingi 2000/-.

5. Mwanakamati atakayepokea rushwa kwa ajili ya kumtorosha mhalifu atapewa faini ya shilingi 30000/.

6. Iwapo afisa mtendaji wa kijiji atashindwa kutekeleza kazi yake baada ya wahalifu kufikishwa kwake na wanakamati atafikishwa katika serikali ya kijiji na kama hakuna utekelezaji ,basi afisa mtendaji wa kijiji atafikikishwa mbele kwa mtendaji wa kata.

SEHEMU C: UTARATIBU WA UTEKELEZAJI:

Utaratibu wa utekelezaji wa utoaji wa vibali na kutoza faini na kutoa maamuzi kwa shughuli zote zinazohusu sheria ndogondogo ni jukumu la kamati ya maliasili.

Serikali ya kijiji itakuwa ndiyo msimamizi mkuu wa shughuli zote za msitu.

Kamati ya maliasili ni kamati ya kudumu ,kamati hii kitaalamu ndiyo meneja wa usimamizi wa msitu. Hata hivyo wajumbe wa kamati wanaweza kusitishwa na kukoma kuwa wajumbe endapo wataonekana kutokufuata maadili ya kamati.

Wajumbe wa kamati ya maliasili watateuliwa au kubadilishwa na serikali ya kijiji na kuidhinishwa na mkutano mkuu wa kijiji.

1. Wanakamati ambao watafanya kazi ya kumkamata mhalifu watazawadiwa asilimia 33.3% na asilimia 66.7% itaingia katika mfuko wa kamati ya maliasili.
2. Ni lazima itolewe stakabadhi ya nambari kwa ada zote, faini zote, na mali zote zitakazotaifishwa .
3. Mwanajamii/kiongozi yeyote wa kijiji cha Kikole anayo mamlaka ya kumkamata mtu yeyote anayefanya kosa kinyume na sheria hizi na kumfikisha katika serikali ya kijiji au kamati ya maliasili.
4. Ni wajibu wa kila mwanakijiji kutoa taarifa ya ukiukwaji wa sheria hizi kwa uongozi wa kijiji.
5. Vibali vyote vitolewe na kamati ya maliasili. Kibali ni lazima kiwe na muhuri wa kamati ya maliasili pia kieleze mahali na muda idadi na kiasi na aina ya mazao hayo.
6. Baada ya mazao hayo kuvunwa na kupimwa kibali kirudishwe kwa kamati ya maliasili.

Sheria hizi zimekubaliwa na kupitishwa kwenye mkutano mkuu wa kijiji na kupitishwa na;

1. Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji.....
2. Afisa Mtendaji wa Kijiji.....
3. Afisa Mtendaji wa Kata (Kwa niaba ya kamati ya maendeleo ya kata).....

Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imekubali sheria hizi katika azimio lililopitishwa kwenye kikao chake cha baraza la madiwani kilichofanyika

Tarehe.....
Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.....

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa…….

KIAMBATANISHO: B

Mpango wa ufuatiliaji shirikishi wa shughuli mbalimbali dhidi ya malengo yaliyowekwa.

Dhumuni	Malengo	Shughuli	Viashiria	Namna ya kuhakiki	Mbinu za kufuatilia	Wahusika	Muda
Kutunza, Kusimamia, na kutumia rasilimali za msitu kiuendelevu kwa ajili ya kuhifadhi bionuai na kuboresha uchumi wa jamii.	Hekta 450 za msitu wa jamii Kijiji cha Kikole zitakuwa zimetunzwa na kusimamiwa kwa kiwango cha wastani wa 80% ifikapo Desemba 2010.	-Kupanda miti ya asili maeneo ya wazi.	Idadi ya miti iliyopandwa	Taarifa ya upandaji wa miti.	Taarifa za mwezi na kutembelea maeneo yaliyopandwa miti.	-Kamati ya maliasili. -Serikali ya kijiji.	Wakati na baada ya kupanda miti.
		-Kufanya doria za mara kwa mara.	Idadi ya matukio ya uhalifu kupungua.	Taarifa za uhalifu.	Kupitia taarifa za doria.	-Kamati ya maliasili. -Serikali ya kijiji.	Kila mwezi
		-Kubabua msitu.	Kuona eneo la msitu lililo babuliwa.	-Matukio ya moto kupungua..	Kutembelea maeneo yaliyobabuliwa.	-Kamati ya maliasili . -Serikali ya kijiji. -Wataalamu.	Msimu wakiangazi unapoanza.
		-Kuanzisha vitalu vya miti.	Vitalu vya miche kuanzishwa.	Taarifa za kuwepo kwa vitalu vya miti.	Kutembelea vitalu vya miti vilivyopo.	-Kamati ya maliasili. -Serikali ya kijiji. -Jamii ya Kikole	Kila baada ya wiki moja baada ya bustani kuanzishwa.
		-Kuweka na kuvitumia vituo vya ukaguziwa mazao ya msitu.	Idadi ya vituo vilivyojengwa.	Kuviona vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu.	Kutembelea vituo vilivyojengwa.	-Kamati ya maliasili. -Serikali ya Kijiji. -Jamii a Kikole	Vituo vikaguliwe kila mwezi.
		-Kusimamia usimamiaji washeria ndogo za kijiji.	Kuwa na kabrasha la sheria ndogondogo zinazotumika.	Kuwa na sheria ndogondogo	Taarifa za kila mwezi.	-Kamati ya maliasili. -Serikali ya kijiji. -Wataalam. -Jamii ya Kikole	Wakati wowote.
		-Kutengen neza barabara za moto.	Urefu na upana na wa babarabara za moto.	Kuonekana kwa barabara.	Taarifa za kila mwezi.	-Kamati ya maliasili. -Serikali ya kijiji. -Jamii ya Kikole.	Kuanzia mwezi wa sita.
		-Kuunda mradi wakutengenez a majiko banifu	Kutengeneza majiko.	Idadi ya majiko banifu yaliyootengene zwa.	Kuyaona majiko	-Kamati ya maliasili. -serikali ya kijiji. -Wataalam. -Jamii	Wakati wote.

Dhumuni	Malengo	Shughuli	Viashiria	Namna ya kuhakiki	Mbinu za kufuatilia	Wahusika	Muda
	Kila kaya kutumia jiko banifu ifikapo mwaka 2010.	-Kuunda mradi wakutengeneza majiko banifu	Kutengeneza majiko.	Idadi ya majiko banifu yaliyootengenezwa.	Kuyaona majiko	-Kamati ya maliasili. -Serikali ya kijiji. -Wataalam. -Jamii ya Kikole	Wakati wote.
		-Kuhamasisha ujenzi wa nyumba za matofali ya kuchoma	Kuonekana nyumba zilizo jengwa kwa tofali za kuchoma.	Tofali za kuchoma kuonekana	Kwa kutembelea na kuona	-Jamii ya Kikole. -Serikali ya kijiji. -Kamatiya maliasili.	Wakati wote.
	Ujenzi wa nyumba za kudumu za gharama nafuu.	Mashamba ya mazao ya kudumu na ya muda mfupi.	Kuonekana kwa mashamba ya kudumu.	Kuyatembelea mashamba.	Kwakutembelea mashamba	-Kamati ya maliasili. -Serikali ya kijiji. -Wataalam. -Jamii ya Kikole	Wakati wote.
	Kuhamasisha kilimo cha kudumu bila kuhama hama.	Kiasi cha mapato yaliyokusanywa.	Kuangalia benki kuna kiasi gani cha Pesa.	Taarifa za pesa zilizo andaliwa.	Ukaguzi wa vitabu vya mapato	-Serikali ya kijiji. -Wataalam. -Jamii ya Kikole	Wakati wote.
	Kukusanya mapato yatokanayo na misitu	Kuundwa kwa vikundi vya miradi midogomidogo.	Kutembelea vikundi.	Kutembelea nakuona vikundi.	Kwa kutembelea.	-Serikali ya kijiji. -Wataalam. -Jamii ya Kikole	Wakati wote.
	Vikundi vya miradi midogomidogo ya kiuchumi.	Kupata mafunzo ya ujasiriamali kuhusu miradi midogo midogo.	Idadi ya washiriki	Kwa kuwahoji washiriki.	Kutembelea sehemu za mafunzo.	-Serikali ya kijiji. -Wataalam. -Jamii ya Kikole	Wakati wote.
	Mafunzo ya ujasiriamali						

KIAMBATISHO: C

Mpango wa kazi wa mwaka katika msitu wa akiba wa kijiji cha Kikole.

Na	Shuguli	Lengo	Muda wa kufanyika kwa shughuli hiyo												Mahitaji	Wahusika	
			J	F	M	A	M	J	J	A	S	O	N	D		Kijiji	Halm a-shauri
1	Kuweka barabara za moto														Vitendea kazi: panga, jembe, shoka, na reki.	✓	
2	Ubabuaji	Kubabua Ha 28													Vitendea kazi: Viberiti, Panga, Wataalamu, Nguvu kazi.	✓	
3	Kukusanya mbegu	4 kg, kwa msimu													Vitendea kazi, mifuko, viroba, Nguvu kazi: jamii	✓	
4	Kuandaa vitalu vya miche.	Miche 6000													Vitendea kazi: Ndoo za kumwagilia, Udongo, Viriba, Nguvu kazi: Jamii, Wataalam.	✓	✓
5	Upandaji wa miti	Miche 6000													Jembe, shoka, Reki, Nguvu kazi; wanakamati, jamii.	✓	
6	Doria	Mara nne kwa mwezi.													Vitendea kazi: Boots, mishale, panga, ovaroli, Koti la mvua.	✓	
7	Kupata mafunzo ya uokotaji wa mbegu.	Washiriki Kamati ya mazingira.													Vitendea kazi; vifaa vya kufundishia, Peni, Daftari,		✓
8	Kujenga kituo cha ukaguzi wa mazao ya msitu.	Kujenga vituo viwili,													Vitendea kazi Panga, jembe, vifaa vya ujenzi. Nguvu kazi; Kamati ya maliasili.	✓	
9	Kusimamia Matumizi ya sheria ndogo.														Vitendea kazi; kabrasha la sheria ndogo, Nguvu kazi; jamii, wanakamati.	✓	
10	Ujenzi wa nyumba za matofali ya kuchoma.	Jamii ya Kikole													Vitendea kazi; Udongo, jembe, Nguvu kazi; jamii	✓	
11	Kupata mafunzo ya Kilimo bora na uvuvi bora.	Jamii ya Kikole.													Vitendea kazi. Madaftari, Kalamu, vifaa vya kufundishia.		✓
12	Kupata mafunzo ya kutengeneza na kutumia majiko banifu.	Jamii ya Kikole													Vitendea kazi. Madaftari, Kalamu, vifaa vya kufundishia. Nguvu kazi: wanakamati, jamii.		✓
13	Kupata mafunzo kuhusu uundaji wa vikundi vidogovidogo vya miradi ya kiuchumi.	Kuanzisha vikundi vine: Nyuki, Ususi, Useremala, na uvuvi.													Vitendea kazi. Madaftari, kalamu, vifaa vya kufundishia, mzinga, nyavu, rangi, misumeno, Nguvukazi.Wanakamati, jamii.		✓